# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeni za Uanaharakati: **Karatasi ya Kazi ya maandalizi ya Kampeni.**

## Utangulizi

Paza Sauti, Chukua Hatua-Sasa! Ongoza Njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake katika Mtandao wa Kanda wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Kampeni ya siku 16 za Uanarakati. Itakayofanyika kuanzia tarehe 25 Novemba hadi tarehe 10 Desemba 2015. Tunakuhimiza kutumia fursa hii kuandaa kampeni yako ya utetezi na kuwahimiza viongozi wenu kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake na wasichana. Huu ni wakati muafaka na fursa ya kushawishi viongozi wa Afrika kuwajibika ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake, na kuwa na umakini zaidi kuhusu masuala ya Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana pamoja na usawa wa kijinsia.

Nia na lengo la karatasi kazi hii ni kupanga, na kufafanua madai yako kwa kutumia kampeni ya kikanda 'Uliza utetezi. Angalizo: kukamilisha karatasi kazi hii inapaswa kuwa shughuli ya kwanza kabisa ya kufanya takribani mwezi mmoja kabla ya kampeni kuanza. Kama una matatizo ya kutumia karatasi kazi hii tafadhali andika kwa kutumia jean@raisingvoices.org kwa msaada.

Mwaka huu tunatoa wito kwa viongozi wetu wote wa kisiasa (mfano wabunge, na viongozi wengine wakuchaguliwa katika ngazi ya Taifa na ngazi ya msingi ya serikali) na viongozi wa Wataalam (kwa mfano Makamishina, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Wafanyakazi na Wataalam katika ngazi ya msingi katika serikali) kwa kutumia sauti zao na kuchukua hatua za kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake.

## Kampeni ya Uliza Utetezi

Kama asasi yako inafanya kazi katika ngazi ya Taifa, kampeni hii hususani inatoa wito kwa viongozi kufanya yafuatayo:

1. Ongea kwa uwazi na hadharani kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake.
2. Kuandaa au kuimarisha mipango ya kitaifa ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.
3. Kuanzisha mfumo wa Uratibu ambao una mamlaka ya kutosha ya kuandaa bajeti, kutekeleza na kufuatilia hatua za kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.
4. Kuhakikisha kwamba fedha za kutosha zimetolewa katika bajeti ili kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.

Kama asasi yako inafanya kazi katika ngazi ya msingi ya serikali yaani mkoa / wilaya / kata / ngazi za chini za mtaa, kampeni hii hususani inatoa wito kwa viongozi kufanya yafuatayo:

1. Ongea kwa u wazi na hadharani kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake.
2. Kuandaa au kuimarisha mipango ya kitaifa ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana katika jamii.

3. Kuhakikisha mkoa / wilaya / kata / mtaa itaanzisha mfumo wa uratibu ambao una mamlaka ya kutosha ya kuandaa, kutekeleza na kufuatilia hatua ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.

## Jinsi ya kutumia Karatasi kazi hii:

1. Karatasi kazi hii imepangwa katika sehemu mbili: kwa asasi zinazofanya kazi katika ngazi ya kitaifa na asasi zinazofanya kazi katika ngazi ya msingi ya serikali / jamii. Tafadhali jibu maswali kwa mujibu wa ngazi ya shirika lako linapofanyia kazi.
2. Andaa mkutano kwa siku 16 za kampeni na wenzako (ikiwezekana mapema kabla ya Novemba 25 mwanzoni mwa kampeni)
3. Toa taarifa kwa wenzako juu ya mpango wa kampeni ya kikanda ya mwaka 2015: Jadili Siku 16 za Kampeni ya uanaharakati na kubalianeni yafuatayo
   a. Je shirika lako lipo katika nafasi ya kushirikisha wadau mbalimbali kutetea baadhi ya mahitaji ya kampeni tajwa hapo juu? Kama ndiyo endelea na hatua ifuatayo hapo chini
4. Ni malengo gani mahususi ya shirika lako katika kampeni hii?
5. Ni hatua gani utachukua ili kufanikisha malengo mahususi?
6. Nini kitakacho ashiria kuwa malengo tajwa hapo juu yamefikiwa?
7. Soma maswali katika karatasi kazi hii
8. Soma, jadili na jibu maswali. Kama unahitaji kufanya marejeo zaidi kubalianeni wapi taarifa kwa kila swali itokayo wapi mfano, Wizara ya Jinsia, idara ya habari, nyaraka za gazeti nk
9. Tafakari kwa makini juu ya mahitaji machache yaliyo ya muhimu ili kuwa na matokeo yenye ufanisi mzuri (unaweza kuamua kuzingatia suala moja)
10. Kubalianeni mfanyakazi yupi ambaye atakusanya taarifa gani kutoka wapi na kwa namna gani.
11. Kubalianeni kuhusu muda maalum wa kutoa taarifa wa vipengele 7 vilivyo tajwa hapo juu.
12. Baada ya kutoa taarifa,boresha kila kipengele ndani ya vitendea kazi kwa taarifa muhimu ulizozipata kwa ajili ya shughuli zako, yaani, majadiliano na vyombo vya habari, moduli ya mafunzo ya vyombo vya habari, matamasha nk.
13. Sasa upo tayari kuanza kampeni yako, tumia sauti yako, chukua hatua na ongoza njia ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake!

## Karatasi Kazi:

### Asasi zote lazima zijibu maswali mawili ya kwanza hapa chini:

1. Ni viongozi gani katika nchi yako wameweza kukemea hadharani juu ya Ukatili Dhidi ya Wanawake?
   a. Jinsi gani mmeweza kutambua juhudi zao, kuwatia moyo kuendelea na kuwashirikisha katika utetezi wenu?
   b. Ni viongozi gani wanaoweza na wanaopaswa kuzungumza zaidi hadharani kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana? Ni namna gani unaweza kuwawajibisha kwa hili?
   c. Fanya tafiti na jumuisha uwajibikaji ambao umesemwa na viongozi kuhusu kuzuia na kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake kwa siku za awali. Ni jinsi gani utawabana viongozi kwa uwajibikaji wa ahadi zao?

d. Fikiria mwenyeji wa majadiliano ya jamii ambapo jamii itawakabili viongozi kuwapa wito kuongea hadharani na kuchukua hatua kwa ajili ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake

2. Ni takwimu zipi zilizopo kuhusu kiwango na athari za Ukatili Dhidi ya Wanawake ikiwa pamoja na gharama za kiuchumi, mzigo katika huduma za afya na athari juu ya elimu kutoka vyanzo vinavyoaminika kama, tafiti za idadi ya watu na afya kitaifa na WHO taarifa ya ufuatiliaji duniani.

## Kwa Mashirika yanayofanya kazi ngazi ya Taifa:

3. Je, nchi yako ina Mpango wa Taifa wa utekelezaji kwa ajili ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake?

> Mipango ya Utekelezaji ya Taifa inaelezwa kama mipango ambayo imeandaliwa ili kufikia lengo kwa mfano, usawa wa kijinsia. Mipango ya utekelezaji hujumuisha muda maalum na tarehe za mwisho, na wakati gani mipango itakuwa tayari kwa kuanza na kwa wakati gani hatua na malengo yatafikiwa.

a. Kama siyo, hatua gani zinatakiwa kutengenezwa katika nchi yako?

b. Kama ndiyo, lakini bado ipo katika rasimu: hatua gani zinatakiwa ili kuikamilisha (tafadhali taja hatua na watu wanaohusika)

c. Kama ndiyo na imekamilika, angalia kama mpango ina vipengele vifuatayo

i. Malengo yanayopimika

ii. Mpango ya kujenga uwezo

iii. Mgawanyo wa bajeti wa kutosha

iv. Kuwepo na uimarisha wa mifumo

v . Ushirikishwaji wa sekta mbalimbali ambazo ni: afya, ustawi wa jamii, polisi, sheria, elimu na jinsia.

vi. Kama kuna kipengele chochote hapo juu kinakosekana je ni mchakato gani wa kuwajumuisha na kuimarisha mpango uliopo?

vii. Watu gani katika ofisi husika wanaweza kuhakikisha mpango wa taifa unakamilika na kuimarishwa?

d. Ni taasisi zipi na watu husika waliomo wanamamlaka ya kuhakikisha mngawanyo wa bajeti kwa kila moja ya sheria na sera hizo?

e. Ni washirika gani, wafuasi na makundi shiriki wanaushawishi wa watu walio tajwa hapo juu? Namna gani (na nani) watashirikiana nao ili kuhakikisha mngawanyo wa bajeti

4. Je, nchi yako ina mfumo wa kitaifa wa uratibu wa kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake?

> Mfumo wa taifa wa uratibu: Unaweza kuwezesha ushirikiano kati ya wizara, asasi za kiraia na vyombo vingine vinavyofanya kazi katika suala husika. Wanauwezo wa kushirikishana kwa taarifa na utekelezaji wa shughuli kwa pamoja. Ni muhimu kuhakikisha mgawanyo bayana wa wajibu na majukumu na kutambua maeneo ya ushirikiano katika utekelezaji wa mikakati na hatua za mipango ya taifa.

a. Je, ni hatua gani zinazohitajika kuanzisha mfumo huo? Kama siyo, tafadhali taja hatua za asasi yako inayohitaji kufanya utetea wa moja wapo (hii itakuwa ni pamoja na wadau wengine)

b. Ni watu gani katika taasisi gani wana mamlaka ya kuanzisha hayo?

c. Kama ndiyo, je mfumo huo una mamlaka na bajeti ya kutosha kufanya kazi kwa ufanisi?

i. Ni taasisi zipi na watu gani maalum ndani ya taasisi wanauwezo wa kuhakikisha mngawanyo wa bajeti kwa kila moja ya sheria na sera hizo?

ii. Washirika gani, wafuasi na makundi mengine wanaushawishi wa watu waliotajwa hapo juu? Namna gani (na nani) watashirikiana nao ili kuhakikisha mgawanyo wa bajeti

5. Je, nchi yako ina sheria maalum na sera ya kushughulikia aina zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake?

> Mifano ya sheria na sera maalum:
> - Afrika Kusini ina sera ya makosa ya kujamiiana ya mwaka 2005
> - Uganda ina sheria ya Ukatili Majumbani ya mwaka 2010
> - Nigeria ina sera ya taifa ya jinsia ya mwaka 2006
> - Algeria ina mkakati wa kitaifa wa mapambano dhidi ya Ukatili Dhidi ya Wanawake

a. Je, sheria na sera zilizotajwa hapo juu zimetekelezwa / zimeshinikizwa kwa ufanisi? Kwa nini ndiyo au kwa nini sio?

b. Utekelezaji / ushinikizwaji wa sheria na sera hizi umetengewa fedha? Kama ndiyo, ni mtiririko gani maalum wa bajeti?

c. Ni mzunguko gani wa bajeti katika nchi yako yaani mchakato na muda kwa ajili ya kutengeneza bajeti za kitaifa au serikali katika ngazi ya msingi?

d. Ni pointi gani ya kuanzia katika shirika lako na washirika / wafuasi wake?

e. Ni taasisi gani na watu maalum ndani wanauwezo wa kuhakikisha mgawanyiko wa bajeti kwa kila moja ya sheria na sera hizo?

f. Ni washirika gani, wafuasi na makundi mengine wanaushawishi juu ya watu waliotajwa hapo juu? Namna gani (na nani) watashirikiana nao ili kuhakikisha mgawanyo wa bajeti?

6 .Ni asasi nyingine zipi zinashiriki katika utetezi sawa kama asasi yako? Je, itachukua muda gani ili kukidhi na kukubaliana maeneo mbalimbali mlio lenga kwa ajili ya ufanisi wa utetezi katika kampeni hii?


GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum Fostering Activism

## Kwa asasi za kiraia zinazofanya kazi katika ngazi za msingi za serikali na mashirika ya kijamii (CBOs)

1. Je, jamii yako ina mpango kwa ajili ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake?
    a. Kama siyo, hatua gani zinatakiwa kutengeneza mpango katika jamii yako?
    b. Kama ndiyo, lakini bado ni katika rasimu: hatua gani zinatakiwa ili kuikamilisha (tafadhali taja hatua na watu wanaohusika)
    c. Kama ndiyo na imekamilika, angalia kama mpango una yafuatayo;
        i. Malengo yanayopimika
        ii. Mpango Kazi
        iii. Mpango wa kujenga uwezo
        iv. Mgawanyo wa bajeti wa kutosha
        v. Kuwepo na uimarisha wa mifumo
        vi . Ushirikishwaji wa sekta mbalimbali ambazo ni: afya, ustawi wa jamii, polisi, sheria, elimu na jinsia.
        vii. Kama kuna kipengele chochote hapo juu kinakosekana je ni mchakato gani wa kuwajumuisha na kuimarisha mpango uliopo?
        viii. Watu gani katika ofisi husika wanaweza kuhakikisha mpango wa jamii unakamilika na kuimarishwa?

d. Ni idara zipi na watu maalum waliomo wana uwezo wa kuhakikisha mngawanyo wa bajeti kwa kila moja ya shughuli na programu?

e. Ni washirika gani, wafuasi na makundi mengine wana ushawishi wa watu walio tajwa hapo juu? Namna gani (ni nani) watashirikiana nao ili kuhakikisha mngawanyo wa bajeti.



GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism